SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

# SERA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR

**2023**

# SERA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA ZANZIBAR

**YALIYOMO**

YALIYOMO ........ i
DIBAJI ........ iii
SHUKURANI ........ iv
UFUPISHO WA MANENO ........ v
TAFSIRI YA MANENO ........ vi
SURA YA KWANZA ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 Usuli ........ 1
1.2 Upeo wa Sera ........ 2
1.3 Uhusiano wa Sera na Miongozo mengine ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa ........ 3
1.3.1 Mikataba ya Kimataifa ........ 3
1.3.2 Mikataba ya Kikanda ........ 4
1.3.3 Sera na Mipango ya Kitaifa ........ 4
1.3.4 Mfumo wa Kisheria ........ 7
**SURA YA PILI ........ 9**
2.0 HALI HALISI ........ 9
2.1 Muundo na mifumo ya kudhibiti na kukabiliana na dawa za kulevya ........ 9
2.2 Matumizi na Athari za Dawa za Kulevya ........ 10
2.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya katika Umri Mdogo ........ 10
2.4 Utegemezi wa Dawa za Kulevya ........ 10
2.5 Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya ........ 11
2.6 Kubadilisha matumizi ya dawa tiba kuwa dawa za kulevya ........ 12
2.7 Utakatishaji wa Fedha Haramu zinazotokana na dawa za kulevya. ........ 12
2.8 Kupunguza athari za matumizi ya dawa za kulevya ........ 12
2.9 Dawa za kulevya na Uharibifu wa Mazingira ........ 14
2.10 Dawa za kulevya na Watu wenye Mahitaji Maalumu na Makundi Maalumu ........ 15
SURA YA TATU ........ 16
3.0 DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA ........ 16
3.1 Umuhimu wa kuundwa kwa sera ........ 16
3.2 Dira ........ 16

3.3 Dhamira ..... 17
3.4 Lengo kuu ..... 17
3.5 Malengo Mahsusi ..... 17
3.6 Kanuni Elekezi za Sera ..... 17
SURA YA NNE ..... 18
4.0 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA ..... 18
Hoja ya Sera 1: Muundo na mifumo isiyojitosheleza katika kudhibiti na kukabiliana na athari za dawa za kulevya. ..... 18
Hoja ya Sera 2: Matumizi na athari ya Dawa za Kulevya ..... 18
Hoja ya Sera 3: Matumizi ya dawa za kulevya katika umri mdogo ..... 19
Hoja ya Sera 5: Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya ..... 20
Hoja ya Sera 6: Kubadilisha Matumizi ya dawa tiba kuwa dawa za kulevya ..... 21
Hoja ya Sera 7: Utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na dawa za kulevya. ..... 22
Hoja ya Sera 8: Kupunguza athari za matumizi ya dawa za kulevya ..... 22
Hoja ya Sera 9 : Dawa za kulevya na Uchafuzi wa Mazingira ..... 23
Hoja ya Sera 10: Dawa za Kulevya na Watu wenye Mahitaji Maalumu na Makundi Maalumu ..... 23
SURA YA TANO ..... 25
5.0 MFUMO YA KITAASISI NA KISHERIA ..... 25
5.1 Mfumo wa kitaasisi ..... 25
5.2 Mfumo wa Kisheria ..... 25
5.3 Majukumu ya wahusika wakuu wa sera ..... 25
SURA YA SITA ..... 29
6.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI ..... 29
6.1 Ufuatiliaji ..... 29
6.2 Tathmini ..... 29
6.3 Mapitio ..... 29
6.4 Gharama na Rasilimali fedha ..... 30
6.5 Mkakati wa Mawasiliano ..... 30

## DIBAJI

Zanzibar inakabiliwa na tatizo la kuongezeka kwa dawa za kulevya ambazo zinaendelea kuwa tishio kubwa kwa afya, usalama na ustawi wa watu wake, hasa kwa vijana na watu wazima. Tatizo la dawa za kulevya huathiri maendeleo endelevu ikiwa ni pamoja na juhudi za kutokomeza umaskini, kutishia usalama wa taifa na kuathiri utii wa sheria. Athari hizi hutokea licha ya juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Matatizo ya dawa za kulevya yamesababisha kuongezeka kwa madhara mbalimbali yakiwemo kuongezeka kwa uhalifu, kupungua kwa nguvu kazi ya taifa hasa vijana, Serikali kutumia gharama kubwa kwa huduma za afya kwa watumiaji wa dawa za kulevya, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza ikiwemo VVU/ UKIMWI, Virusi vya Homa ya Ini (B na C) na Kifua Kikuu (TB), kuporomoka kwa maadili miongoni mwa vijana na vifo vinavyosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya.

Kutokana na ongezeko la dawa za kulevya na athari zinazoendelea kuikumba jamii, ni muhimu sana kuwepo kwa Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambayo itatoa muongozo katika kudhibiti upatikanaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya Zanzibar. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeandaa Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya itakayoweka muongozo juu ya udhibiti wa usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Aidha, Sera hii itabadilisha mtazamo kwa watoaji wa huduma za afya, wasimamizi na watekelezaji wa sheria na mawakala wengine kuhakikisha kuwa watumiaji wa dawa za kulevya, wanapatiwa huduma mbadala na kuhamasisha uzingatiaji wa haki za binaadamu badala ya kuadhibiwa.

**..................................**

**Harusi Said Suleiman**
**Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**
**Zanzibar.**

## SHUKURANI

Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar imeandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Sera hii inatokana na michango muhimu iliyotolewa na wadau tofauti na mashirika kutoka ndani na nje ya Zanzibar. Nachukua nafasi hii adhimu kuwashukuru wataalamu wote kwa michango yao muhimu. Shukurani za dhati ziende kwa taasisi mbalimbali ambazo kwa njia moja au nyengine zilishiriki katika kufanikisha uandaaji wa Sera hii muhimu ya taifa. Tunalishukuru Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa msaada wao wa kifedha katika kuandaa Sera hii.

Aidha, shukurani zetu za dhati ziende kwa taasisi ambazo ziliwaruhusu wafanyakazi wao kushiriki katika kuandaa Sera hii. Taasisi hizo zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Uratibu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana Dawa za Kulevya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar, Wizara inayoshughulikia masuala ya Katiba na Sheria, Wizara inayoshughulikia masuala ya Wanawake na Watoto, Wizara inayoshughulikia masuala ya Afya, Wizara inayoshughulikia masuala ya Elimu na Wizara inayoshughulikia masuala ya Kilimo. Taasisi nyengine ni pamoja na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Shirika la Bandari Zanzibar na ZAYEDESA. Kwa kuwa sio rahisi kumtaja mtu mmoja mmoja, natoa shukurani kwa wale wote ambao kwa njia moja au nyengine wameshiriki katika kukamilisha sera hii.

…………………………

**Dkt. Omar Dadi Shajak**
**Katibu Mkuu**
**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**
**Zanzibar.**

## UFUPISHO WA MANENO

| | |
|---|---|
| MAT | Medically Assisted Treatments |
| MKKDK | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya |
| SADC | Southern African Development Community (Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika) |
| TB | Tuberculosis (Kifua Kikuu\|) |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | United Nations Programme Development (Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa) |
| UNODC | United Nations Office on Drugs and Crime (Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani) |
| VVU | Virusi Vya UKIMWI |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan 2026 (Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar) |
| ZAYEDESA | Zanzibar Youth Education, Enviroment Support Association |
| ZIHTLP | Zanzibar Intergrated HIV, Tubeculosis and Lepsory Program (Programu ya Pamoja ya VVU, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar) |

## TAFSIRI YA MANENO

**Dawa haramu** - ni dawa zote zinazofanyakazi kwenye ubongo ambazo hutumika kwa ajili ya kubadilisha hisia, fikra au tabia bila madhumuni halali ya tiba na ambazo hazijapitishwa na sheria kwa ajili ya matumizi katika nchi husika.

**Kasumba** - ni dawa ghafi zote zenye uasili wa kufanya kazi kwenye ubongo na kuleta mabadiliko katika hisia, mtazamo, kisaikolojia au ya kitabia kama ilivyoainishwa katika Muongozo wa I na II wa Mikataba ya Dawa za Kulevya ya 1961 kama ilivyorekebishwa na Itifaki ya 1974.

**Kemikali bashirifu** - ni kemikali zinazotumika kutengezea dawa za kulevya visivyo halali na kinyume cha sheria.

**Marekebisho ya tabia** - ni mkusanyiko wa shughuli zilizoundwa ili kurahisisha utaratibu wa kumtoa mtu katika matumizi na utegemezi wa dawa za kulevya ili kumuunganisha tena kwenye jamii.

**Sober houses** – ni nyumba za upataji nafuu kwa walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya.

**Usafirishaji wa dawa za kulevya (Trafficking)** - ni shughuli inayofanywa na mtu yeyote katika kuingiza ama kutoa dawa za kulevya katika nchi husika ama katika eneo husika.

**Utakatishaji wa fedha haramu** - ni kitendo cha mtu au watu kujihusisha moja kwa moja au kwa njia nyengine katika kupokea, kusindika, kuficha, kudanganya, kubadilisha, kugeuza, kuharibu, kuondoa au kuleta katika nchi husika fedha au mali ambazo zinaaminika kuwa ni pato la uhalifu (kama uhalifu wa dawa za kulevya).

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Usuli

Zanzibar ina visiwa vikuu viwili, Unguja na Pemba ambapo mbali ya visiwa hivyo pia vipo visiwa vyengine vidogo vidogo vinavyoishi watu ikiwemo kisiwa cha Tumbatu na Uzi, kwa upande wa Unguja na kisiwa cha Kojani, kisiwa Panza, Fundo, Uvinje, Kokota, Shamiani Mwambe na Makoongwe kwa upande wa Pemba. Pia vipo visiwa vyengine vidogo visivyoishi watu. Zanzibar ipo katika bahari ya Hindi kilomita 30 kutoka pwani ya Afrika ya Mashariki, kati ya nyuzi yalatitude 5 na 7 kusini mwa Ikweta. Zanzibar ina eneo la kilomita za mraba 2,654 ambapo Unguja ina eneo la kilomita za mraba 1,666 na Pemba ina kilomita za mraba 988 (*Zanzibar Statistical Abstract, 2021*). Zanzibar ina idadi ya watu wapatao 1,889,773 (915,492 ni wanaume na wanawake ni 974,281). Kasi ya ongezeko la idadi ya watu ni wastaani wa asilimia 3.7 hali inayoifanya Zanzibar kuwa ni miongoni mwa nchi zenye ukuaji mkubwa wa idadi ya watu katika nchi za Afrika ya Mashariki (Sensa ya Watu na Makaazi 2022).

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zilizoathirika na tatizo la dawa za kulevya ambapo karibu mikoa yote mitano imeathirika na tatizo hilo ikiongozwa na Mkoa wa Mjini Magharibi unaoripotiwa kuongoza kwa kuwa na kesi nyingi za dawa za kulevya. Jumla ya kesi za dawa za kulevya zilizoripotiwa Zanzibar katika kipindi cha miaka minne (2019 - 2022) ni 1,819. Kati ya hizo kesi zilizoripotiwa katika Mkoa wa Mjini Magharibi ni 911, Mkoa Kusini Unguja 294, Kaskazini Unguja 269, Kusini Pemba 232 na Kaskani Pemba 113. Kesi hizo zilihusisha dawa za kulevya zenye uzito wa jumla ya kilogramu 1334.46 ambapo heroini kilogramu 22.5, bangi kilogramu 1,257.25, mirungi kilogramu 51.13, valiamu kilogramu 1.4 na kokeni kilogramu 2.18. (Ripoti za Hali Halisi ya Dawa za Kulevya Zanzibar za mwaka 2019 - 2022).

Aidha kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika Mkoa wa Mjini Magharibi kunakoambatana na idadi kubwa na mchanganyiko wa wakaazi kunakadiriwa kupelekea kuongezeka kwa shughuli za usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Hii inaonesha uwepo wa haja ya kuimarisha zaidi mikakati ya mapambano ya dawa za kulevya hasa katika maeneo yaliyoathirika zaidi.

Serikali imechukua hatua mbali mbali katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Miongoni mwa jitihada hizo ni kutungwa na kupitishwa Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nambari 8 ya mwaka 2021 iliyoanzisha Mamlaka yenye dhamana ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya, kuanzisha vituo vya tiba na marekebisho ya tabia na kuanzisha programu za kuelimisha jamii kuhusu madhara ya dawa za kulevya.

Serikali inashiriki kikamilifu katika vikao vya Kitaifa na Kimataifa ili kuimarisha juhudi za kupunguza na kuondoa uhalifu unaotokana na dawa hizo. Pamoja na jitihada kubwa za kudhibiti uhalifu wa dawa za kulevya zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali bado tatizo hili linaendelea kuiathiri jamii ya Zanzibar. Hali hii inathibitishwa kwa kuwepo na matatizo mengi ya kiafya, kijamii na kiuchumi yanayotokana na athari ya matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Jitihada za haraka zinahitajika ili kukabiliana au kuondoa tatizo la dawa hizo kwa lengo la kukuza ustawi wa jamii**.** Juhudi zote hizi zimekuwa zikifanyika bila ya kuwa na sera inayosimamia udhibiti na mapambano ya dawa za kulevya Zanzibar.

Kuwepo kwa Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kutatoa muongozo wa kitaifa wa kukabiliana na changamoto za usafirishaji pamoja na tatizo la matumizi ya dawa hizo, kwa kusaidiana na sera nyengine za kisekta zinazohusiana na kukabiliana na dawa za kulevya na masuala ya kiafya na kijamii. Sera hii pia, itafafanua na kubainisha masuala muhimu yanayohusiana na tatizo la dawa za kulevya, kuonesha dhamira ya nchi katika kuhakikisha ustawi wa jamii kwa ujumla, na kuimarisha, kukuza na kuongeza nguvu za kupambana na dawa za kulevya ikiwemo kupunguza mahitaji na madhara ya dawa hizo. Sera hii itasaidia kuanzishwa kwa mifumo imara ya udhibiti wa dawa za kulevya.

### 1.2 Upeo wa Sera

Sera hii itatumika katika maeneo yote ya Zanzibar na itahusika na masuala ya dawa za kulevya ikijumuisha uzalishaji wa dawa za kulevya, udhibiti wa usafirishaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, itatoa fursa ya ushirikiano katika utekelezaji wa mikakati ya sera na itifaki za kikanda, pamoja na mikataba ya kimataifa inayohusiana na dawa za kulevya. Walengwa wa sera hii ni Serikali na taasisi zake, asasi za kiraia, washirika wa maendeleo na jamii kwa ujumla.

## 1.3 Uhusiano wa Sera na Miongozo mengine ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa

Sera imezingatia miongozo ya mikataba ya kimataifa, itifaki za kikanda, kitaifa na kisekta inayohusiana na masuala ya dawa za kulevya zikiwemo:

### *1.3.1 Mikataba ya Kimataifa*

**Mkataba wa Mihadarati wa mwaka 1961, (*The Single convention on Narcortic Drugs,1961*) kama ulivyorekebishwa na Itifaki ya mwaka 1972.**

Malengo makuu ya mkataba huo ni kupunguza umiliki, utumiaji, biashara, kusambaza, kuingiza, kusafirisha, kutengeneza na kuzalisha dawa za kulevya, isipokuwa kwa madhumuni ya tiba na shughuli za kisayansi na kushughulikia biashara ya dawa za kulevya kupitia ushirikiano wa kimataifa ili kuwazuia na kuwadhibiti wahalifu wa dawa za kulevya.

**Mkataba wa Dawa Tiba zinazofanyakazi katika ubongo (The Convention on Psychotropic substance) wa mwaka 1971.**

Mkataba huu ulianzisha mfumo maalumuu wa Kimataifa wa kudhibiti matumizi ya dawa tiba zinazofanyakazi kwenye ubongo. Mkataba huu unatoa ufafanuzi wa kutokukengeuka kwa matumizi halisi ya dawa tiba na kuweka wigo mpana wa udhibiti wa dawa zote zilizotengenezwa kiwandani ambazo zina nguvu sawa katika kutibu na kuweza kuathiri iwapo zitatumika vibaya.

**Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Usafirishaji wa Dawa za Kulevya na kutumia Dawa Tiba zinazofanyakazi kwenye ubongo (Psychotropic) wa mwaka 1988.**

Mkataba huu umeweka misingi madhubuti dhidi ya usafirishaji wa dawa za kulevya ikiwemo kuweka miongozo dhidi ya ukengeukaji wa kemikali bashirifu (precursor chemicals). Mkataba huo umetoa msisitizo wa ushirikiano wa Kimataifa, kwa mfano kubadilishana wahalifu wa dawa za kulevya na udhibiti wa usafirishaji na mapato ya uhalifu wa dawa hizo.Mkataba huo unawanyima wahalifu wa dawa za kulevya fursa za kujipatia fedha na uhuru wa kusafiri, kupanua wigo wa udhibiti ili kuzuia utakatishaji wa fedha chafu na haramu na kufuatilia kwa karibu, kuzuia na kutaifisha mali zinazotokana na uhalifu wa dawa za kulevya.

**Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto 1989**

Mkataba huu unaelezea hatua za kisheria, kiutawala, kijamii na kielimu ili kuwalinda watoto dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya kama ilivyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa, pamoja na kuwalinda watoto wasitumike katika uzalishaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.

### *1.3.2 Mikataba ya Kikanda*

**Itifaki ya Kupambana na Dawa haramu katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) 1996.**

Itifaki hii ilijumuisha mikataba ya kimataifa ambayo nchi wanachama walikubaliana kuwepo miongozo ya sheria za ndani ya nchi na kuwepo ushirikiano wa pamoja wa masuala ya sheria na utekelezaji wenye ufanisi. Itifaki hii pia inashajihisha nchi wanachama kuanzisha mpango wa kupunguza matumizi ya dawa za kulevya na mipango maalumuu itakayoleta ufanisi wa kudhibiti rushwa.

**Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Uhalifu wa Dawa za Kulevya katika Kanda ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2001.**

Itifaki hii ililenga kuilinda kanda hiyo isitumike kama sehemu ya kupitishia dawa za kulevya kuelekea mataifa ya nje, kudhibiti uzalishaji wa dawa za kulevya, usafirishaji, utakatishaji wa fedha haramu na matumizi mabaya ya dawa tiba kwa kushirikiana na wasimamizi wa sheria na kupunguza mahitaji kupitia uratibu wa programu za kikanda.

### *1.3.3 Sera na Mipango ya Kitaifa na Kimataifa*

**Dira ya Dunia ya Maendeleo Endelevu (SDG’s)**

Lengo namba 3 la Dira ya Dunia ya Maendeleo Endelevu (SDG’s) linalohusiana na Afya na Ustawi kwa makundi yote limekusudia, pamoja na mambo mengine, kuimarisha huduma za kinga na tiba kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

**Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050**

Dira ya 2050 lengo nambari 2.5.9 (**A**spiration Nam. 2.5.9) inaelezea kuwepo kwa viwango

endelevu vya uidhinishaji na ufuatiliaji wa matibabu ya matumizi ya dawa za kulevya yenye kusaidia tafiti na teknolojia husika ili kupunguza matumizi ya dawa za kulevya na dawa nyengine zenye athari kama dawa za kulevya.

**Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026 (ZADEP)**

Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021- 2026 umezingatia masuala ya dawa za kulevya katika kifungu 3.5.5.1 kinachoelezea hifadhi ya jamii (social protection) ambapo vipengele nambari iii na ix vinaelekeza kuwepo na mfumo kamili wa utoaji huduma kwa jamii, unaojumuisha makundi mbalimbali wakiwemo waathirika wa matumizi ya dawa za kulevya kwa kuimarisha vituo vya utoaji huduma za marekebisho ya tabia na kuweka viwango bora vya utambuzi na ufuatiliaji wa matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya.

**Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 -2025**

Ibara ya 196 (a-g) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 -2025 imezungumzia kuhusu biashara na utumiaji wa dawa za kulevya kuwa ni janga kwa jamii, jinsia na rika zote hivyo, udhibiti wake ni jambo muhimu kwa ustawi wa taifa**.**

**Mpango Mkakati wa Kitaifa wa VVU NA UKIMWI – Zanzibar 2022**

Mpango Mkakati wa Kitaifa wa VVU-Zanzibar unasisitiza utekelezaji wenye umuhimu wa kuzuia VVU/UKIMWI ambao hushajihisha kupunguza hatari ya maambukizo kwa njia ya mabadiliko ya tabia kati ya makundi maalumuu wakiwemo watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidungasindano.

**Sera ya Afya ya Akili, 1998**

Sera hii imekusudia kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, ikiwemo kuratibu mipango ya afya ya akili na utegemezi wa dawa za kulevya ili kutoa huduma kwa wale wenye maradhi pacha (afya ya akili na matumizi ya dawa za kulevya) na kulinda haki za binadamu na kuwa karibu katika uangalizi wa mapato na mali za walengwa.

**Sera ya Elimu, 2006**

Sera hii inatambua kuwa matumizi ya vilevi miongoni mwa vijana sio tu kuwa yanaharibu afya zao lakini pia ni chanzo cha kutoweka kwa nidhamu na kuwepo kwa vurugu katika skuli. Vile vile, wanafunzi ambao hutumia dawa za kulevya mara nyingi hutoroka skuli na hatimaye huwa kwenye hatari ya kuambukizwa virusi vya UKIMWI. Sera hii inasisitiza uwepo wa programu madhubuti

za kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na vilevi vyengine katika ngazi ya skuli.

**Sera ya Afya, 2011**

Sera ya Afya imeonesha kuwa miongoni mwa sababu zinazopelekea ongezeko la maambukizo ya ugonjwa wa UKIMWI ni pamoja na matumizi ya dawa za kulevya.

**Sera ya Taifa ya VVU/ UKIMWI – Zanzibar, 2012**

Sera hii inatambua kuwa watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga sindano wako katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU/UKIMWI na kuweka mikakati ya kuanzisha na kutekeleza programu za matumizi salama ya bomba za sindano ili kuepuka maambukizi mapya kwa wanaojidunga sindano, kuanzisha vituo vya utoaji sumu na marekebisho ya tabia kwa kutumia huduma ya tiba saidizi (methadone). Sera inasisitiza programu za kuwashajihisha watuamiaji wa dawa za kulevya waweze kuzitumia huduma zinazopatikana katika vituo vya afya na vituo vya marekebisho ya tabia. Aidha, sera imebainisha kuwa asilimia 26 ya watumiaji wa dawa za kulevya wanaojidunga sindano wamepata maambukizi ya maradhi ya kujamiiana kilinganishwa na asilimia 0.3 tu ya maambukizi ya ujumla katika jamii.

**Sera ya Serikali za Mitaa Zanzibar, 2014**

Sera hii imetambua kuwa tatizo la dawa za kulevya ni tishio kwa ustawi wa jamii hasa kwa vijana na kudhoofisha maendeleo ya watu wa Zanzibar, pia huzorotesha mafanikio katika juhudi za kupunguza umasikini na kuleta mvurugiko wa kisaikolojia na akili.

**Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar, 2014**

Sera hii imetilia mkazo uanzishwaji wa nyumba za marekebisho ya tabia zitakazotoa huduma za makaazi, matibabu na mafunzo kwa waathirika wa dawa za kulevya pamoja na kushajiihisha uanzishwaji wa nyumba salama zitakazotoa huduma kwa wanawake wanaotumia dawa za kulevya.

**Sera ya Msaada wa Kisheria, 2017**

Sera ya msaada wa kisheria imehusisha masuala ya msaada wa kisheria katika utoaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa makundi yenye mahitaji maalumu, katika haki ya kupata msaada wa kisheria kwa maskini na wenye mahitaji maalumu ambayo inajumuisha watumiaji wa dawa za kulevya.

**Sera ya Michezo, 2018**

Sera ya Michezo inaeleza kuwa utumiaji wa dawa za kulevya umekuwa ukikatiza ndoto za vijana wengi ambao walitamani kuwa wachezaji bora ambao watalitangaza taifa ndani na nje ya nchi. Wanamichezo wengi wamejingiza katika matumizi ya dawa za kulevya na kuacha vipaji vyao vikipotea. Sera hii imeweka mikakati ya kukinga na kupiga marufuku matumizi na usambazaji wa dawa za kulevya kupitia programu za michezo pamoja na kushajihisha vijana kushiriki katika michezo kama kinga ya kujiepusha na utumiaji wa dawa za kulevya.

**Sera ya Watu wenye Ulemavu, 2018.**

Sera ya Watu wenye Ulemavu inatambua uhusiano wa matumizi ya dawa za kulevya na matukio ya ulemavu. Sera imebainisha miongoni mwa vyanzo vikuu vya kupata ulemavu ni ulevi na matumizi ya dawa za kulevya.

**Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, 2022**

Sera hii imezingatia masuala mtambuka ambayo yanajumuisha mahitaji na fursa za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinazozingatia watu wenye mahitaji maalumu wakiwemo waathirika wa dawa za kulevya. Sera hii imehamasisha uanzishwaji wa programu za uwezeshaji zinazotoa fursa za ushiriki wa makundi yote wakiwemo watu wenye mahitaji maalumu, na kuweka mazingira wezeshi kwa programu zitakazotoa fursa za ajira na kuondoa tatizo la ajira nchini hasa kwa watu wa makundi maalumu.

**Sera ya Maendeleo ya Vijana, 2023**

Sera ya Maendeleo ya Vijana imetambua umuhimu wa kushiriki na kuwashirikisha vijana wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu katika shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, imeweka mikakati maalumu ya kuanzisha program za uwezeshaji kiuchumi kwa vijana wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu ili waweze kujitambua na kuepukana na vitendo vitakavyohatarisha afya ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya.

### *1.3.4 Sheria mbalimbali*

Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inatambua kuwepo kwa sheria na kanuni zinazodhibiti na kukabiliana na ukuaji wa tatizo la usambazaji na upunguzaji wa matumizi ya

dawa za kulevya Zanzibar, baadhi ya sheria hizo ni :-

**Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nam. 8 ya mwaka 2021**

Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nam. 8 ya mwaka 2021 imezingatia hoja za kisera ambazo ziliibuliwa sambamba na mapitio ya Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nam.9 ya mwaka 2009. Sheria hii ilipitishwa kukabiliana na tatizo la dawa ya kulevya, ambayo inatekeleza mikataba ya Kimataifa inayokataza ulimaji, umiliki, utumiaji, usindikaji, uzalishaji, uandaaji, uuzaji, ununuaji, usambazaji, uhifadhi, uingizaji na usafirishaji wa Dawa za kulevya nje na ndani ya Zanzibar.

Hii ni kutokana na msukumo wa kisiasa uliokuwa na dhamira ya kuimarisha msingi wa kisheria ili kuongeza nguvu katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Mbali na kuwa mamlaka, Taasisi ya Dawa za Kulevya imeimarishwa na inaendelea kuimarishwa kwa kupatiwa watumishi na vitendea kazi vinavyohitajika katika utekelezaji wa majukumu yake

**Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu Nam. 10 ya mwaka 2009**

Sheria ya Kupambana na Utakatishaji wa Fedha Haramu na Mapato yanayotokana na Uhalifu ya mwaka 2009 katika kifungu cha 2 imefafanua kuwa makosa ya dawa za kulevya ni miongoni mwa makosa makubwa yanayohusiana na utakatishaji wa fedha haramu. Sheria hii ina uwezo wa kufuatilia mali na mapato yote ya wahalifu na hatimaye kuzuia na kutaifisha mali hizo.

**Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Nam 1 ya mwaka 2012**

Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Nam 1 ya Mwaka 2012 katika kifungu cha 50 imeanzisha kosa la usafirishaji wa dawa za nakotiki na saikotropiki kwa njia yoyote kinyume na sheria.

**Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Nam. 2 ya mwaka 2006**

Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya Mwaka 2006 katika kifungu cha 78 kimezingatia baadhi ya dawa tiba kuwa ni dawa za kulevya pia katika kifungu cha 79 kimepiga marufuku, uzalishaji, uingizaji, uuzaji wa dawa yoyote inayodhibitiwa kwa matumizi ya matibabu au matumizi ya kisayansi isipokuwa iwe imefuata masharti ya sheria.

**Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Nam.10 ya mwaka 2011**

Sheria ya Uanzishaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, katika kifungu 5 kinaelezea kuhusu uchunguzi na upimaji wa dawa za kulevya pamoja na kutoa ripoti ya mwisho ya matokeo ya uchunguzi wa dawa za kulevya.

**Sheria ya Kukinga na Kudhibiti VVU na UKIMWI Nam. 18 ya mwaka 2013**

Sheria hii ilitungwa kwa lengo la kutoa kinga na kudhibiti maambukizi ya VVU / UKIMWI Zanzibar, kwa ajili ya kukinga na kuimarisha haki za binadamu kwa watu wanaoishi na VVU na masuala yao ya maisha ya kila siku. Sheria hii katika kifungu cha 5 (1) (2) imeipa jukumu Tume ya UKIMWI ya kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na sababu, athari na njia za kujikinga VVU na UKIMWI kwa watu wa makundi maalumu yanayojumuisha watumiaji wa dawa za kulevya.

### *1.3.5 Muundo wa Kitaasisi*

Masuala ya dawa za kulevya yanasimamiwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar. Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ndiye msimamizi wa kisera kuhusiana na dawa za kulevya. Kitaifa lipo Baraza la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambalo linaongozwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya unahusisha pia vyombo vyengine muhimu katika kusimamia haki jinai ikiwemo Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkemia Mkuu wa Serikali na Jeshi la Polisi. Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa zimepewa majukumu ya kushughulikia masuala ya dawa za kulevya katika maeneo yao ya kiutawala. Changamoto inayoendelea kuzikabili jitihada za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya ni pamoja na ushirikiano mdogo wa taasisi zinazohusika. Sera hii inaweka misingi kwa taasisi zote na mtu mmoja mmoja kushiriki kikamilifu katika mapambano ya dawa za kulevya.

# SURA YA PILI

## 2.0 HALI HALISI

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC - 2021) inakadiriwa kuwa zaidi ya watu milioni 275 wenye umri wa miaka 15-64 duniani kote wanatumia dawa za kulevya. Kati ya hao, watu Milioni 36.3 wanakabiliwa na tatizo la utegemezi wa dawa za kulevya.

Zanzibar kama zilivyo nchi nyengine duniani inakabiliwa na tatizo la uingizaji, usambazaji na matumizi dawa za kulevya. Takwimu za kesi za dawa za kulevya kwa Zanzibar ni kama ifuatavyo:- kwa kipindi cha miaka minne (2019 – 2022) jumla ya kesi za dawa za kulevya zilizoripotiwa ni 1,819 ( 1,474 Unguja na 345 Pemba).

Mwenendo wa kesi za dawa za kulevya unaonesha kwamba mwaka 2020 kesi za dawa za kulevya zimepungua kwa asilimia 9.7 ikilinganishwa na mwaka 2019 (kesi 503 mwaka 2019 hadi kesi 454 mwaka 2020). Aidha idadi ya kesi imeongezeka katika mwaka 2021 kwa asilimia 21 (kutoka kesi 454 mpaka kesi 550) na mwaka 2022 idadi ya kesi zimepungua kwa asilimia 44 (kutoka kesi 550 mpaka kesi 312) (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar). Pamoja na kupanda na kushuka kwa kesi za dawa za kulevya hali halisi mitaani inaonesha athari za dawa za kulevya zinaonekana kushamiri katika jamii.

### *2.1 Muundo na mifumo ya kudhibiti na kukabiliana na dawa za kulevya*

Muundo na mifumo iliyopo katika kudhibiti dawa za kulevya inaonekana kutokidhi mahitaji yanayoendana na mbinu zinazotumika katika usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Suala la udhibiti wa dawa za kulevya linahitaji utendaji madhubuti. Hata hivyo bado inaonesha kuwa kuna upungufu unaojumuisha, ushirikiano usiotosheleza baina ya taasisi zinazosimamia masuala ya dawa za kulevya, baadhi ya wasimamizi wa sheria kukosa uadilifu na uaminifu, uhaba wa rasilimali watu na utaalamu usiotosheleza katika kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya. Vilevile, uhaba wa vitendea kazi unaojumuisha majengo ya ofisi na vituo vya huduma, kukosekana kwa Sheria inayohusiana na fedha haramu na jamii kuwa na muhali wa kutoa taarifa za uhalifu katika maeneo yao wanayoishi ni miongoni mwa changamoto zinazopelekea kukosekana ufanisi katika kukabiliana na dawa za kulevya.

### *2.2 Matumizi na Athari za Dawa za Kulevya*

Matumizi ya dawa za kulevya yanasababisha athari mbalimbali zikiwemo mifarakano ya kifamilia kutengwa na jamii, mmong'onyoko wa maadili na kutelekezwa kwa watoto. Aidha, usalama wa jamii pia umekuwa hatarini kwa kuwa watumiaji wengi wanajihusisha na vitendo vya uhalifu ikiwemo wizi, magenge ya uporaji, ubakaji na uharibifu wa mali na miundombinu.

Watumiaji wa dawa za kulevya wapo katika hatari ya kupata maradhi mbali mbali yakiwemo ugonjwa wa mapafu, akili, moyo, utegemezi wa dawa za kulevya, shindikizo la damu na maambukizi ya VVU/UKIMWI na homa ya Ini B na C. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya kwa kiwango kikubwa yanaendelea kusababisha maradhi sugu hasa miongoni mwa wanaojidunga sindano na vifo vya ghafla.

Matumizi ya dawa za kulevya yanasababisha uzalishaji mdogo wa kipato unaotokana na kupungua nguvu kazi ya taifa, hali inayopelekea kupunguza pato la taifa na la familia ambalo linatumika zaidi kuwahudumia na kuwatibu watumiaji wa dawa za kulevya. Pamoja na kuwepo kwa athari za wazi zinazotokana na matumizi ya dawa za kulevya bado hakuna tafiti rasmi zinazotoa idadi halisi ya watumiaji wa dawa za kulevya nchini.

### *2.3 Matumizi ya Dawa za Kulevya katika Umri Mdogo*

Taarifa zinaonesha kwamba kwa sasa utumiaji wa dawa za kulevya unaanza katika umri mdogo ukilinganisha na miaka iliyopita. Tabia ya kuanza matumizi ya dawa za kulevya katika umri mdogo inaashiria uwepo wa utegemezi wa muda mrefu ukilinganisha na wale wanaoanza kutumia katika umri mkubwa. Imeripotiwa kuwa matumizi ya dawa za kulevya huanza kwa watoto wenye umri kati ya miaka 9 – 13, (ZIHTLP – 2019). Sababu zinazochangia kuanza matumizi ya dawa za kulevya katika umri mdogo ni pamoja na shinikizo rika, ukosefu wa stadi za maisha, athari za utandawazi, ukosefu wa malezi ya pamoja katika jamii na mfarakano wa familia.

### *2.4 Utegemezi wa Dawa za Kulevya*

Tatizo la utegemezi wa dawa za kulevya linasababisha matatizo makubwa katika jamii, licha ya ukweli kwamba tatizo hilo linaweza kukingwa na kutibika. Kwa mujibu wa Ripoti ya Hali ya Dawa za Kulevya Zanzibar 2020 jumla ya waathirika 9,854 walipatiwa huduma ya upataji nafuu kwa kipindi cha miaka 10 ( 2012 -2022). Kati ya waathirika hao 5,123 (52%) walirudia matumizi ya

dawa za kulevya. Utegemezi wa dawa za kulevya unatokana na sababu mbalimbali zinazopelekea kurudia matumizi ya dawa za kulevya. Uhaba wa huduma zinazosaidia kupata nafuu kwa wategemezi wa dawa, kukaa kwa muda mfupi katika vituo vya tiba, kutokua na shughuli za kiuchumi baada ya kupata nafuu na kutengwa na familia na jamii ni miongoni mwa sababu kuu za kurudia matumizi ya dawa za kulevya.

### *2.5 Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya.*

Jiografia ya visiwa vya Zanzibar ni changamoto kubwa katika mapambano dhidi ya usafirishaji wa dawa za kulevya kutokana na kuwepo katika ukanda wa Kusini mwa Bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC) nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini zinatajwa kuwa ni miongoni mwa njia za kupitishia dawa za kulevya aina ya heroini zinazotoka Afghanistani na kuelekea Asia, Mashariki ya Kati, Ulaya na Marekani. Aidha harakati na tabia za kihalifu za kibinadamu zimechangia upatikanaji wa dawa nyengine ikiwa ni pamoja na bangi, mirungi na kokeni.

Usafirishaji wa dawa za kulevya hapa Zanzibar umekuwa ukifanyika katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandari rasmi na zisizo rasmi pamoja na madiko. Hii inatokana na uhaba wa vifaa vya kisasa vya upekuzi na uchunguzi, kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya doria vyenye uwezo wa kukabiliana na vyombo vinavyotumika katika usafirishaji dawa za kulevya (baharini) usimamizi wa madiko usiotosheleza pamoja na taaluma isiyotosheleza katika masuala ya uchunguzi na upekuzi.

Ripoti ya Polisi ya Kitengo cha Kupambana na Dawa za Kulevya imeonesha kwamba kipindi cha mwaka 2012-2021, jumla ya kesi za dawa za kulevya zilizoripotiwa ni 4,146 ambapo jumla ya kilo 42.22 za heroini, kilo 2,143.9 za bangi, kilo 169.32 za mirungi, kilo 54.8 za kokeni na kilo 3,946 za valiamu zilikamatwa.

Zanzibar ina bandari bubu zaidi ya 371 ambazo pia zimekuwa ni kichocheo kikubwa cha usafirishaji wa dawa za kulevya. Aidha, usafirishaji wa dawa za kulevya huathiri ukuaji uchumi na kusababisha kuwepo kwa utakatishaji wa fedha haramu, mfumko wa bei na rushwa.

Katika kuendelea na mapambano ya udhibiti wa dawa za kulevya, moja ya mbinu zinazotumika kuzuia uzalishaji na upatikanaji wa malighafi zinazotokana na kemikali bashirifu, ambapo bila

kuwepo kemikali hizo dawa za kulevya haziwezi kuzalishwa. Hata hivyo kemikali bashirifu muhimu zimekuwa zikitumika katika viwanda halali. Licha ya matumizi makubwa yanayokubalika, kemikali bashirifu zinaweza kuwa hatari endapo zitabadilishwa matumizi yanayokubalika na kuenda katika matumizi ya utengenezaji wa dawa za kulevya. Ukosefu wa taaluma ya kugundua haraka kemikali bashirifu kwa watendaji, unatoa mwanya kwa waingizaji wa magendo wa kemikali hizo kuingiza katika nchi kwa kukwepa taarifa sahihi zinazohitajika katika taratibu za usafirishaji kwa kubadilisha lebo au kuweka lebo ya kughushi katika makontena yanayoingizwa.

### *2.6 Kubadilisha Matumizi ya Dawa Tiba kuwa Dawa za Kulevya*

Kumekuwa na ongezeko la matumizi mabaya ya dawa tiba zilizo chini ya udhibiti wa kisheria kutumika kama dawa za kulevya hasa dawa zenye kusababisha usingizi zikiwemo *valium, cetrizine, piriton na morphine.* Watumiaji wa dawa za kulevya wanatumia dawa hizo kama dawa za kulevya. Ubadilishaji wa matumizi halali ya dawa tiba unafanyika kwa njia mbalimbali na kushirikisha wahalifu wa aina tofauti. Katika kuzipata dawa hizo watumiaji wa dawa za kulevya wanashirikiana na watoa huduma za afya kama; matabibu ikijumuisha madaktari wa meno, madaktari wa wanyama, wafamasia, wauguzi, na wafanyakazi wengine kuwapatia wahalifu dawa hizo.

### *2.7 Utakatishaji wa Fedha Haramu zinazotokana na Dawa za Kulevya.*

Mtiririko wa fedha nyingi upo katika mikono ya wahalifu wa usafirishaji wa dawa za kulevya. Matumizi ya fedha hizo yanakuwa na madhara makubwa kwa uchumi wa ndani na nje. Fedha zinaweza kuhamishiwa nje ya nchi kwa kununua au kujenga mali isiyoweza kuhamishika, na kuwekeza katika mikahawa na majumba ya kuchezesha kamari kwa ajili ya kutakatisha au kuficha fedha hizo katika taasisi zisizotoa taarifa za kifedha.

### *2.8 Kupunguza Athari za Matumizi ya Dawa za Kulevya*

**Huduma za Upataji Nafuu:** Huduma za upataji nafuu zinalenga kuwatoa watu katika utegemezi wa dawa za kulevya na kupunguza athari za kiafya, kijamii na kiuchumi zinazotokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa mtu mmoja mmoja, familia na jamii kama ifuatavyo:- Serikali imewapatia mafunzo ya huduma ya upataji nafuu kwa kutumia hatua 12, walioacha matumizi ya dawa za

kulevya jambo lililopelekea kuanzishwa nyumba za upataji nafuu (sober houses), kuanzishwa kwa kituo cha Serikali cha tiba na marekebisho ya tabia Kidimni, kuanzishwa programu ya kutumia tiba saidizi, programu za ujasiriamali kwa walioathirika na kusaidia huduma za upataji nafuu zinazotolewa na asasi za kiraia na watu binafsi.

**Matibabu na marekebisho ya tabia:** Katika kuhakikisha upatikanaji wa matibabu kwa watumiaji wa dawa za kulevya, huduma mbalimbali za marekebisho ya tabia zenye lengo la kuwatoa watu katika utegemezi wa dawa za kulevya na kuwarudisha katika hali ya kawaida zinaendelea kutolewa. Miongoni mwa huduma hizo ni ushauri nasaha, kutolewa sumu mwilini, tiba za mabadiliko ya tabia na kujitambua, matibabu ya dharura, kuhamasishana na kusaidiana katika makundi rika. Huduma hizo zimekuwa zikitolewa katika taasisi tofauti pamoja na nyumba za upataji nafuu maarufu kama "Sober house". Mfumo wa nyumba hizi umeanzishwa hapa Zanzibar mwaka 2009 ambao hujikita zaidi na matibabu ya muongozo wa hatua 12.

Katika kipindi cha 2012-2022, nyumba za upataji nafuu zilihudumia watumiaji 9,854 kwa Unguja na Pemba. Ripoti inaonesha kwamba watumiaji wanawake ni 384 (4%) na wanaume 9,470 (96%). Waatumiaji hao walikuwa na umri wa miaka 18 na kuendelea. Taarifa ya mafanikio ya Nyumba za Upataji Nafuu kwa pipindi cha mwaka 2012 - 2022 ni kuwa watu 3,362 (34%) waliohudumiwa walifanikiwa kuacha kabisa matumizi ya dawa za kulevya, watu 5,123 (52%) wamerudia matumizi ya dawa za kulevya, watu 381 (4%) walibadilisha utumiaji wa dawa za kulevya kutoka kwenye heroini kwenda kwenye kilevi chengine na watu 988 (10)% hakuna taarifa zao (Taarifa ya Mwaka ya Hali Halisi ya Dawa za Kulevya 2022). Pamoja na huduma hizo bado inaonekana kuwepo haja ya kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa watumiaji wa dawa za kulevya na programu za kuzuia ongezeko la watumiaji wapya.

Imebainika kwamba mafanikio bora yanafikiwa pale mbinu jumuishi zilizo na wigo mpana zenye mchanganyiko wa taaluma za tiba na saiklojia kama vile matibabu ya kuacha matumizi ya dawa za kulevya, huduma za kimatibabu, ushauri nasaha, upataji nafuu, maisha baada ya tiba na maarifa ya kujitegemea yanayomuwezesha mtumiaji wa dawa za kulevya kukabiliana na mazingira tofauti. Dhana ya kwamba utumiaji wa dawa za kulevya ni tabia ya kujitakia inayohitaji mtu kuadhibiwa, inapelekea kwa kiasi kikubwa hukataliwa kupewa huduma. Aidha, imebainika kuwa mbinu za kutibu na kuzuia matumizi kwa watumiaji wa dawa za kulevya kupitia adhabu kali hushindwa kwa

sababu hazizingatii mabadiliko ya kibaiolojia ambayo yamesababishwa na utegemezi wa dawa hizo.

**Matibabu ya kutumia tiba saidizi:** Huduma ya matibabu ya kutumia tiba saidizi imethibitika kuwaponya wategemezi wa heroini kwa kuanzishwa huduma ya dawa ya methadoni. Huduma hiyo inasimamiwa na Wizara ya Afya na inaendeshwa katika Kliniki ya Methadoni iliyopo katika Hospitali ya watu wenye matatizo ya afya ya akili Kidongo Chekundu. Huduma hiyo imeanza kutolewa mwaka 2015 na imelenga kuwasaidia watumiaji wa heroini kupunguza athari za matumiziya dawa hiyo kwa Zanzibar. Kufikia Disemba 2022, jumla ya watumiaji 1551 (wanaume 1471, wanawake 80) walisajiliwa katika kliniki hiyo. Kati ya hao watumiaji 39 (wanaume 36, wanawake 3) wamefanikiwa kuacha matumizi ya dawa za kulevya na watumiaji 926 (wanaume 881, wanawake 45) wanaendelea na huduma na kuhudhuria kliniki kila siku.

**Kuunganishwa tena na jamii baada ya kupata nafuu:** Mpango wa kuunganisha vijana waliokuwa wakitumia dawa za kulevya na jamii baada ya kupata nafuu ni kipimo kinachoonesha mafanikio kwa kiasi fulani. Kupitia nyumba za upataji nafuu hutolewa mafunzo ya amali yanayowawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali wanaporudi katika jamii pamoja na kupatiwa mafunzo ya kompyuta kwa ajili ya uendeshaji wa kazi za kila siku. Huduma baada ya upataji nafuu ambayo inawasaidia vilivyo kubaki katika usalama wa kibaiolojia, kisaikolojia na shughuli za kijamii zinazowashajihisha kuwa katika maisha mazuri. Hata hivyo hali ilivyo hivi sasa inaonesha hakuna mazingatio ya kutosha ya kuwawezesha waliopata nafuu wanaporudi kukubalika katika jamii. Jitihada zaidi za Serikali na taasisi binafsi zinahitajika katika kuwawezesha kiuchumi waliopata nafuu ili kufikia lengo la kuwarejesha kikamilifu katika jamii na kufaidika na fursa zilizopo.

### *2.9 Dawa za kulevya na Uharibifu wa Mazingira*

Shughuli zinazohusiana na matumizi ya dawa za kulevya huchangia ongezeko la uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Baadhi ya kemikali zinazotumika kutengenezea dawa zina asili ya miripuko na sumu. Mabaki ya bidhaa yanayozalishwa mara nyingi hutupwa mwituni, maeneo ya wazi, kwenye michirizi ya maji na kwenye mito na kusababisha hasara kubwa za kimazingira. Vilevile, utupaji ovyo wa mabomba ya sindano zinazotumika kujidunga na vifaa vyengine vinavyotumika katika natumizi ya dawa za kulevya husababisha uharibifu wa mazingira.

### *2.10 Dawa za kulevya na Watu wenye Mahitaji Maalumu na Makundi Maalumu*

Watu wenye mahitaji maalumu na makundi maalumu wanakabiliwa na changamoto katika kupata huduma za upataji nafuu dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya zinazotolewa kwa jamii ambao wanajumuisha makundi ya watoto, wanawake, waathirika wa VVU na UKIMWI, wajawazito, Watu wenye ulemavu na walio katika hali duni ndani ya jamii. Vile vile baadhi ya wahalifu wengine wamekuwa wakiwatumia watoto na watu wenye ulemavu katika usambazaji wa dawa za kulevya jambo ambalo linaleta matatizo makubwa kwa familia za makundi hayo pamoja na kuharibu ustawi wa maisha yao.

Jitihada nyingi zinazochukuliwa katika kukabiliana na athari za dawa za kulevya zimeonekana kujikita kwa watumiaji wanaume na hazijazingatia watumiaji wanawake, hivyo hupelekea kundi hili kutofaidika ipasavyo na huduma zinazotolewa kwa watumiaji na waathirika wa dawa za kulevya ikiwemo uanzishwaji wa nyumba maalumu za upataji nafuu kwa ajili ya wanawake wanaotumia na walioathirika na dawa za kulevya.

## SURA YA TATU

## 3.0 DIRA, DHAMIRA NA MALENGO YA SERA

### 3.1 Umuhimu wa kuundwa kwa sera

Tatizo la dawa za kulevya linaathiri kwa kiasi kikubwa jamii ya Zanzibar. Dawa za kulevya zimekuwa zikisababisha matukio ya ajali mbalimbali za barabarani pamoja na kusababisha ulemavu na vifo. Udhibiti wa dawa za kulevya umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uhaba wa vifaa vya kisasa vya upekuzi na uchunguzi, utaalamu usiotosheleza katika masuala ya uchunguzi na upekuzi wa dawa za kulevya, mifumo ya kudhibiti na kukabiliana na athari za dawa za kulevya isiyojitosheleza na ushirikiano mdogo wa kitaasisi katika udhibiti wa dawa za kulevya. Vilevile, kuna changamoto za uwepo wa bandari bubu na madiko mengi yanayoweza kutumika kupitishia dawa za kulevya, matumizi mabaya ya dawa tiba kuwa dawa za kulevya, utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na usafirishaji wa dawa za kulevya na jamii kuwa na muhali katika kuripoti matukio ya dawa za kulevya.

Serikali imekuwa ikichukua jitihada mbalimbali kudhibiti matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya Zanzibar miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi. Jitihada hizi zinaendelea kufanyika bila ya kuwa na sera inayosimamia udhibiti wa dawa za kulevya. Sera hii itatoa muongozo utakaoelekeza mbinu na kuweka mikakati imara ya udhibiti pamoja na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya, itaimarisha usimamizi, uratibu na ushirikiano na itasaidia kurahisisha utekelezaji wa moja kwa moja katika ngazi zote kuanzia jamii hadi taifa katika kudhibiti dawa za kulevya. Sera hii pia itakuwa ni utekelezaji wa matakwa ya Mikataba ya Kimataifa na Itifaki za Kikanda inayohusiana na udhibiti wa dawa za kulevya.

### 3.2 Dira

Kuwa na jamii iliyoepukana na dawa za kulevya ili kuhifadhi nguvu kazi ya taifa kwa maendeleo ya Zanzibar.

### 3.3 Dhamira

Kudhibiti usafirishaji, usambazaji, utengenezaji, matumizi na kupunguza athari za dawa za kulevya kiafya, kijamii na kiuchumi kwa kuanzisha na kuimarisha utekelezaji wa mifumo ya kisheria, kitaasisi, programu, uhamasishaji jamii na mashirikiano yanayolenga mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

### 3.4 Lengo kuu

Lengo kuu la Sera ni kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya Zanzibar.

### 3.5 Malengo Mahsusi

i. Kuimarisha mifumo na miundo ya kitaasisi katika kukabiliana na uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya;
ii. Kuimarisha na kuendeleza programu zinazohusiana na huduma za tiba, marekebisho ya tabia na kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa mtumiaji na jamii; na
iii. Kuimarisha mashirikiano ya kisekta, kikanda na kimataifa katika kudhibiti na kukabiliana na athari za dawa za kulevya.

### 3.6 Kanuni Elekezi za Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar

Kanuni elekezi zinawakilishwa na

i. Majibu yenye ushahidi;
ii. Uratibu na Mashirikiano;
iii. Ufanisi na Tija;
iv. Mwelekeo wa kitaifa na utekelezaji wenye kuzingatia mipaka ya kimamlaka;
v. Uwazi na Uwajibikaji;
vi. Udhibiti wa taarifa na siri.

## SURA YA NNE

## 4.0 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA

***Hoja ya Sera 1: Muundo na mifumo isiyojitosheleza katika kudhibiti na kukabiliana na athari za dawa za kulevya.***

Mifumo na muundo iliyopo katika kudhibiti dawa za kulevya inaonekana bado haikidhi mahitaji yanayoendana na mbinu zinazotumika katika usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Ufanisi katika kudhibiti dawa za kulevya na athari zake kunahitaji jitihada za pamoja. Hata hivyo bado inaonesha kuwa kuna upungufu katika mifumo na miundo katika usimamizi wa masuala ya dawa za kulevya.

**Tamko la Sera.**

*Serikali itaimarisha muundo na mifumo ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya.*

**Mikakati ya Sera**

i. Kuweka mifumo imara ya kudhibiti na kupambana na dawa za kulevya itakayoleta ufanisi katika kukabiliana na mbinu zinazotumika katika usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya katika ngazi zote;
ii. Kuimarisha uratibu na kusimamia miongozo ya utendaji kazi wa pamoja kwa taasisi na wahusika katika kudhibiti dawa za kulevya; na
iii. Kuimarisha mifumo ya kuhifadhi taarifa za dawa za kulevya.

**Hoja ya Sera 2: Matumizi na athari ya Dawa za Kulevya**

Imeonekana kuongezeka matumizi ya dawa za kulevya hali inayopelekea athari mbalimbali kwa jamii na taifa kwa ujumla na kusababisha kupungua kwa nguvu kazi na pato la Taifa, kuongezeka uhalifu na mmong'onyoko wa maadili.

***Tamko la Sera:*** *Serikali itahakikisha inadhibiti matumizi na athari za dawa za kulevya*.

**Mikakati ya Sera**

i. Kuelimisha jamii kuhusu athari za dawa za kulevya;
ii. Kuimarisha programu za ujasiriamali na mafunzo ya amali kwa vijana waliorekebishwa

tabia;

iii. Kushajihisha vijana kushiriki katika shughuli za kiuchumi, michezo na utamaduni;

iv. Kushajihisha wasanii kutojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo ya michezo na burudani;

v. Kusimamia sheria zinazohusiana na makosa ya uzururaji (vagrancy laws); na

vi. Kuimarisha huduma za tiba na marekebisho ya tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya.

**Hoja ya Sera 3: Matumizi ya dawa za kulevya katika umri mdogo**

Licha ya juhudi zinazochukuliwa kukinga matumizi ya dawa za kulevya katika jamii bado kuna vijana wanaojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya wakiwa katika umri mdogo. Imeonekana kuwa, watumiaji wa dawa za kulevya huanza utumiaji katika umri mdogo kwa miaka ya sasa ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Sababu zinazochangia kuanza matumizi ya dawa za kulevya katika umri mdogo ni pamoja na shindikizo rika, athari za mitandao ya kijamii, malezi mabaya, mfarakano wa kifamilia, hali ya kipato cha familia na ukosefu wa stadi za maisha.

**Tamko la Sera:**

*Serikali itaweka taratibu za kuwalinda na kuwakinga watoto na matumizi ya dawa za kulevya.*

**Mikakati ya utekelezaji:**

i. Kuimarisha programu maalumuu zitakazojumuisha elimu kwa jamii juu ya kujitambuakwa watoto, kuwajengea uwezo na taaluma ya malezi bora;

ii. Kuimarisha programu za stadi za maisha kwa watoto na vijana zitakazowakinga kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya;

iii. Kuimarisha programu za kujenga familia imara katika jamii; na

iv. Kuzishirikisha taasisi za kidini katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

**Hoja ya Sera 4: Utegemezi wa dawa za kulevya**

Tatizo la utegemezi wa dawa za kulevya linatokana na sababu tofauti ikiwemo utumiaji wa dawa za kulevya kwa muda mrefu linalopelekea kurudia matumizi ya dawa za kulevya. Tatizo la utegemezi haliwezi kutibika kupitia adhabu kali badala yake tatizo hili hutibika kupitia programu zinazozingatia mabadiliko ya kibaiolojia yaliyosababishwa na utegemezi wa dawa hizo.

**Tamko la Sera**

*Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za matibabu, marekebisho ya tabia na huduma baada ya kupata nafuu ili kuwalinda waliopata nafuu wasirudie matumizi ya dawa za kulevya.*

**Mikakati ya utekelezaji**

i. Kuimarisha huduma za matibabu ya kuondoa utegemezi wa dawa za kulevya;
ii. Kujenga uwezo wa taasisi na vituo vinavyotoa huduma za tiba na marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya;
iii. Kuimarisha na kuendeleza utekelezaji wa sera, itifaki, mikataba ya kikanda na ya kimataifa ya utoaji wa huduma ili kupata viwango bora vya matokeo ya tiba za utegemezi wa dawa za kulevya;
iv. Kuwezesha upatikanaji wa fursa za uwezeshaji kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya; na
v. Kuhamasisha jamii kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya ikiwemo maambukizi ya VVU/UKIMWI na maradhi mengine yanayoambukizwa kwa njia ya damu.

**Hoja ya Sera 5: Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya**

Usafirishaji wa dawa za kulevya unaongezeka siku hadi siku hususan katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na madiko. Hii inatokana na uhaba wa vifaa vya kisasa vya upekuzi na uchunguzi, usimamizi wa madiko usiotosheleza na utaalamu usiotosheleza katika masuala ya uchunguzi na upekuzi wa dawa za kulevya. Biashara ya dawa za kulevya inahitaji mikakati ya usimamizi wa sheria, isiishie katika kukamata dawa tu, pia ilenge kudhibiti viwanda, mitambo na malighafi za kutengenezea dawa hizo kwa kuweka taratibu za kufuatilia mienendo ya usambazaji na utengenezaji wa dawa za kulevya.

**Tamko la sera**

*Serikali itaimarisha mifumo, miundombinu na upatikanaji wa vifaa katika udhibiti wa usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya katika maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na madiko.*

**Mikakati ya Sera**

i. Kuimarisha ulinzi na operesheni shirikishi na endelevu juu ya kudhibiti usafishirishaji wa dawa za kulevya katika vituo vya usafiri nchini zikiwemo viwanja vya ndege, bandari rasmi na zisizo rasmi pamoja na madiko**;**
ii. Kuwajengea uwezo wasimamizi wa sheria katika maeneo ya kitaalamu ili kukabiliana na vitendo vya usafirishaji wa dawa za kulevya;
iii. Kuhakikisha usimamizi madhubuti wa viwanda, maabara na watumiaji wa kemikali bashirifu;
iv. Kushajihisha jamii kutojiingiza katika shughuli za uzalishaji wa dawa za kulevya;
v. Kutekeleza makubaliano ya kisheria katika ngazi ya Kikanda na Kimataifa katika kupambana na usafirishaji wa dawa za kulevya; na
vi. Kuhakikisha shughuli za uwekezaji hazichangii katika uingizaji, usambazaji na utumiaji.

**Hoja ya Sera 6: Usimamizi wa Sheria**

Kumekuwa na changamoto katika usimamizi wa sheria zinazohusiana na ukamataji, ukusanyaji wa ushahidi na utunzaji wa vielelezo, uendeshaji wa kesi, utoaji ushahidi, utoaji wa adhabu na taratibu za rufaa katika kesi za dawa za kulevya.

**Tamko la Sera:**

*Serikali itahakikisha inaimarisha mfumo wa usimamizi wa sheria katika kusimamia kesi za dawa za kulevya.*

**Mikakati ya Sera:**

i. Kushajihisha mageuzi ya mfumo jinai utakaorahisisha uendeshaji, usimamizi na adhabu kwa kesi za dawa za kulevya;
ii. Kuimarisha mifumo ya kisheria na miundombinu ya uhifadhi na udhibiti wa vielelezo vya kesi za dawa za kulevya, ukamataji, upatikanaji na utoaji ushahidi;
iii. Kutunga sera ya adhabu itakayoelekeza ambayo, pamoja na mambo mengine itafanya mazingatio ya adhabu zinazotolewa kuhusiana na uhalifu wa dawa za kulevya;
iv. Kuweka kwa mifumo ya sheria inayoweka utaratibu wa adhabu mbadala kwa watumiaji wa dawa za kulevya;
v. Kuanzisha mahakama maalumu ya dawa za kulevya na kurahisisha mwenendo wa kesi katika Mahakama;

vi. Kuimarisha taratibu za ukataji rufaa kwa kesi za dawa za kulevya;

vii. Kupitia na kuimarisha sheria zinazohusiana na uendeshaji mashtaka na utoaji adhabu kwa wahalifu wa dawa za kulevya;

viii. Kuanzisha programu za kujenga uelewa kwa jamii kushiriki katika hatua za kukusanya na kutoa ushahidi wa kesi za dawa za kulevya; na

ix. Kuanzisha jukwaa la haki jinai katika kusimamia kesi za dawa za kulevya.

**Hoja ya Sera 7: Kubadilisha Matumizi ya dawa tiba kuwa dawa za kulevya**

Watumiaji wa dawa za kulevya hutumia dawa tiba hasa zenye kusababisha usingizi kama mbadala wa dawa za kulevya hupatikana kinyume na utaratibu wa kitaalamu.

**Tamko la Sera:**

*Serikali itaimarisha mfumo wa usimamizi wa uingizaji na usambazaji wa dawa tiba na matumizi yanayoendana na sheria*.

**Mikakati ya Utekelezaji**

i. Kuimarisha utaratibu wa ndani wa uingizaji na usambazaji wa dawa tiba na zile zinazofanya kazi kwenye ubongo;

ii. Kusimamia utekelezaji wa matumizi sahihi ya mfumo wa kimataifa wa makadirio ya dawa tiba, kemikali bashirifu na zile zinazofanya kazi kwenye ubongo;

iii. Kukuza uelewa kwa jamii juu ya athari ya matumizi ya dawa tiba kinyume na malekezo ya wataalamu;

iv. Kuanzisha mfumo wa kuwaorodhesha na kuwatambua walioruhusiwa kuingiza na kusambaza dawa tiba zilizodhibitiwa; na

v. Kuimarisha mfumo utakaowezesha kufahamu viwango vya dawa tiba vinazoingizwa na kutumika kama dawa za kulevya.

**Hoja ya Sera 8: Utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na dawa za kulevya.**

Utakatishaji wa fedha haramu zinazotokana na usafirishaji wa dawa za kulevya na matukio mengine ya kihalifu, unaendelea kuwa tatizo kubwa la Kimataifa linalotishia usalama na utengamano wa taasisi na mifumo ya fedha kwa kudhoofisha ufanisi, ustawi wa kiuchumi na mifumo ya kiutawala.

**Tamko la Sera:**

*Serikali itaweka mifumo bora ya ushirikiano,utakaowezesha mamlaka husika kuzuia na kutaifisha mali zinazohusishwa na makosa ya dawa za kulevya.*

**Mikakati ya Utekelezaji**

i. Kuvijengea uwezo vyombo vya usimamizi wa sheria vinavyopambana na dawa za kulevya na utakatishaji wa fedha haramu;
ii. Kuweka mifumo ya kisheria itakayodhibiti chumo haramu linalotokana na uhalifu wa dawa za kulevya; na
iii. Kuimarisha uhusiano na kuhakikisha utekelezaji wa itifaki na mikataba ya kikanda na kimataifa juu ya utakatishaji wa fedha haramu.

**Hoja *ya Sera 9: Kupunguza athari za matumizi ya dawa za kulevya.***

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanahitaji uwepo wa mikakati imara ya kupunguza athari za matumizi ya dawa za kulevya ili kuhakikisha watumiaji wa dawa za kulevya wanapata nafuu kutokana na athari za kiafya na mabadiliko ya tabia yanayotokana na utumiaji wa dawaza kulevya na kuunganishwa tena na jamii.

**Tamko la Sera:**

*Serikali itahakikisha inapunguza athari za matumizi ya dawa za kulevya*

**Mikakati ya Utekelezaji**

i. Kuimarisha na kuendeleza programu za huduma za tiba na upataji nafuu;
ii. Kuimarisha vituo vya upataji nafuu;
iii. Kushajiisha jamii kutumia huduma zinazotolewa katika vituo vya upataji nafuu;
iv. Kuimarisha na kuendeleza matumizi ya matibabu ya tiba saidizi kwa watumiaji wa dawa za kulevya;
v. Kuwajengea uwezo waraibu wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya ili kumudu maisha yao; na
vi. Kushajihisha jamii kuwakubali waraibu waliopata nafuu baada ya kuunganishwa tena na familia.

**Hoja ya Sera 10: Dawa za kulevya na Uchafuzi wa Mazingira**

Shughuli za ulimaji, utengenezaji wa dawa za kulevya katika maabara, wakati wa uteketezaji, utupaji ovyo wa bomba, sindano na vifaa nyengine huchangia uchafuzi wa mazingira.

**Tamko la Sera:**

*Serikali itadhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na dawa za kulevya.*

**Mikakati ya Utekelezaji**

i. Kuimarisha usimamizi mzuri wa taka zinazotokana na mabaki ya vifaa vya matibabu vinavyotumiwa na watumiaji wa dawa za kulevya ikiwemo sindano na bomba; na
ii. Kuweka mazingira wezeshi na salama katika kuteketeza dawa za kulevya.

**Hoja ya Sera 11: *Dawa za Kulevya na Watu wenye Mahitaji Maalumu na Makundi Maalumu***

Watu wenye mahitaji maalumu wanakabiliwa na changamoto katika kupata huduma zinazotolewa kwa jamii. Makundi hayo yanajumuisha watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, watoto, vijana walio katika mazingira magumu, wanawake, Watu wenye Ulemavu, wajawazito, watu wenye matatizo ya afya ya kiakili na walio katika hali duni ndani ya jamii. Huduma zinazotolewa kwa waathirika wa dawa za kulevya hazijazingatia ipasavyo mahitaji ya makundi hayo.

**Tamko la Sera:**

*Serikali itahakikisha upatikanaji wa huduma kwa watu wenye mahitaji maalumuu na makundi maalumu walioathirika na dawa za kulevya.*

**Mikakati ya Utekelezaji**

i. Kuweka taratibu zitakazohakikisha kuwa watu wenye mahitaji maalumu, walioathirika na dawa za kulevya wanapata huduma za tiba na marekebisho ya tabia kwa kuzingatiamahitaji yao;
ii. Kuimarisha huduma zikiwemo za kinga, tiba, marekebisho ya tabia na huduma nyengine saidizi zenye mikakati ya kuhudumia makundi maalumuu;
iii. Kujenga uwezo kwa jamii kuanzisha na kuendeleza utoaji huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya na wenye mahitaji maalumu; na
iv. Kuweka utaratibu wa kuwawezesha kiuchumi waathirika wa dawa za kulevya

walioacha matumizi ya dawa za kulevya.

# SURA YA TANO

# 5.0 MFUMO YA KITAASISI NA KISHERIA

## 5.1 Mfumo wa kitaasisi

Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya itasimamiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya dawa za kulevya.

## 5.2 Mfumo wa Kisheria

Ili kupata ufanisi katika utekelezaji wa sera hii baadhi ya mifumo ya kisheria itahitaji kufanyiwa mapitio na marekebisho ili kuendana na dhamira ya sera. Miongoni mwa sheria ambazo zitahitaji kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Nam. 8 ya mwaka 2021, Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Nam.10 ya mwaka 2011 na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Zanzibar Nam. 2 ya mwaka 2006

## 5.3 Majukumu ya wahusika wakuu wa sera

Mafanikio ya utekelezaji wa Sera hii yatafikiwa kwa kuwepo mashirikiano na taasisi na wahusika mbali mbali. Sera hii inatambua wahusika muhimu pamoja na majukumu yao kama ifuatavyo;

**Wizara, Idara na Taasisi (MDAs)**

Wizara, idara na taasisi zote za Serikali zina wajibu wa kuhakikisha kuwa afya, ustawi na uchumi wa watu wa Zanzibar unaimarika kwa kupunguza usambazaji na matumizi ya dawa za kulevya. Ili kufikia lengo hili hakuna budi kwa wizara, idara na taasisi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa sera hii.

**Wizara yenye dhamana na masuala ya dawa za kulevya**

i. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera;
ii. Kufanya ufatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa sera;
iii. Kufanya uchunguzi na udhibiti wa dawa za kulevya;
iv. Kusimamia programu za marekebisho ya tabia;
v. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu dawa za kulevya; na

vi. Kuratibu tafiti zinazohusu masuala ya dawa za kulevya.

**Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa**

i. Kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na athari ya dawa za kulevya;
ii. Kushirikiana na taasisi mbali mbali kuunga mkono shughuli za waraibu walioacha dawa za kulevya;
iii. Kuhamasisha jamii kutumia sanaa ya maonesho katika kufikisha ujumbe wa madhara ya dawa za kulevya; na
iv. Kuhakikisha kamati za ulinzi na usalama za mikoa, wilaya na shehia zinashiriki kikamilifu kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya.

**Wizara inayohusika na uwezeshaji**

i. Kuwajengea uwezo wa ujasiriamali watumiaji wa dawa za kulevya waliomo katika programu za marekebisho ya tabia; na
ii. Kusaidia shughuli zinazofanywa na waraibu walioacha matumizi ya dawa za kulevya.

**Wizara inayohusika na masuala ya Afya**

i. Kuhakikisha usambazaji salama wa dawa na vifaa tiba;
ii. Kuanzisha mfumo wa kuhifadhi taarifa sahihi za usambazaji wa dawa na vifaa tiba; na
iii. Kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa tiba.

**Wizara inayohusika na masuala ya michezo na burudani**

i. Kuimarisha viwanja vya michezo na maeneo ya burudani ili kuwavutia vijana kushiriki katika michezo na burudani;
ii. Kuelimisha wanamichezo na vikundi vya burudani kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya;
iii. Kuandaa programu za michezo zitakazowashajihisha vijana kushiriki michezo ili kuacha kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya; na
iv. Kuviimarisha vikundi vya burudani katika kujipatia kipato katika kazi za ubunifu.

**Wizara za Kisekta**

Wizara za kisekta kutoa ushirikiano katika maeneo yao ya utendaji na wizara yenye dhamana na masuala ya dawa za kulevya.

**Baraza la Taifa la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya**

i. Kutoa maelekezo juu ya uendeshaji wa masuala ya dawa za kulevya; na

ii. Kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Sera.

**Taasisi inayosimamia masuala ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.**

i. Kusimamia na kufuatilia ipasavyo masuala ya rushwa kwa taasisi zinazosimamia udhibiti wa dawa za kulevya; na
ii. Kudhibiti vitendo vya utakatishaji wa fedha haramu.

**Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mahkama.**

i. Kufuatilia na kukamata wahalifu wa dawa za kulevya na makosa yanayohusiana na hayo;
ii. Kuimarisha mashirikiano ya kitaasisi;
iii. Kupeleleza na kuendesha kesi za dawa za kulevya kwa wakati;
iv. Kusikiliza kesi za dawa za kulevya na kuzitolea uamuzi kwa wakati; na
v. Kuhifadhi na kulinda vielelezo vya dawa za kulevya.

**Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali**

Kuimarisha mbinu za uchunguzi wa kimaabara kwa vielelezo vya kesi za dawa za kulevya zitakazowezesha kutoa hati ya uchunguzi kwa muda mfupi.

**Taasisi inayosimamia masuala ya Dawa na Vipodozi**

i. Kudhibiti uingizaji na usalama wa dawa tiba zinazodhibitiwa (controlled substances); na
ii. Kushauriana na taasisi inayosimamia sera hii wakati wa utoaji wa vibali vya uingizaji wa dawa tiba zinazodhibitiwa, kemikali na kemikali bashirifu.

**Shirika la Bandari, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani**

i. Kufanya upekuzi wa dawa za kulevya wakati wa ukaguzi wa abiria na mizigo katika

maeneo ya bandari na viwanja vya ndege;

ii. Kubuni mbinu mbadala za kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya katika viwanja vya ndege na bandari; na
iii. Kuajiri wataalamu wa kutosha watakaoweza kutumia vifaa vya kisasa vya upekuzi wa dawa za kulevya.

**Taasisi za Elimu**

i. Kutoa mafunzo ya athari za matumizi ya dawa za kulevya kwa walimu na wanafunzi wa ngazi zote;
ii. Kuanzisha klabu za kupinga matumizi ya dawa za kulevya katika taasisi za elimu; na
iii. Kutoa elimu ya stadi za maisha kwa vijana.

**Taasisi zinazohusiana na uwekezaji na utalii**

i. Kuhakikisha wawekezaji na watalii wanaoingia nchini hawajihusishi na uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya; na
ii. Taasisi zinazohusiana na utoaji wa vibali vya uwekezaji zinashirikiana na vyombo vyenye dhamana ya udhibiti wa dawa za kulevya.

**Vyombo vya Habari**

i. Kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya dawa za kulevya;
ii. Kuandika habari za kiuchunguzi za kesi za dawa za kulevya.

**Washirika wa Maendeleo**

i. Kusaidia shughuli za kuzijengea uwezo taasisi zinazofanya kazi za uchunguzi wa dawa za kulevya.
ii. Kuchangia juhudi za Serikali katika kutekeleza mikakati ya udhibiti wa dawa za kulevya.

**Sekta binafsi, Jumuiya zisizo za kiserikali, Jumuiya za kiraia na Jumuiya za kidini**

i. Kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kutoa elimu juu ya athari za dawa za kulevya kwa jamii.
ii. Kushajihisha jamii kuwa mstari wa mbele katika kutoa taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya.

iii. Kuchangia na kutoa misaada katika utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa dawa za kulevya.

**Vyama vya Siasa**

i. Kuunga mkono juhudi za Serikali katika kupambana na dawa za kulevya.
ii. Kujumuisha masuala ya dawa za kulevya katika ilani za vyama vya siasa na kufatilia utekelezaji wake.

**Jamii**

i. Kutoa taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya;
ii. Kushiriki kikamilifu katika programu za kukuza uelewa juu ya athari za dawa za kulevya pamoja na huduma za tiba kwa waathirika wa dawa za kulevya; na
iii. Kusaidia vyombo vya ulinzi na usalama katika ukamataji wa wahalifu wa dawa za kulevya.

## SURA YA SITA

## 6.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ili itekelezwe kwa ufanisi itategemea mfumo madhubuti wa ufatiliaji na tathmini. Wizara yenye dhamana na masuala ya udhibiti wa dawa za kulevya itakuwa na jukumu la kutayarisha mfumo wa ufatiliaji na tathmini. Mfumo wa ufatiliaji na tathmini wa Sera hii itatekelezwa kwa kuzingatia mfumo uliotayarishwa na Tume ya Mipango Zanzibar.

### 6.1 Ufuatiliaji

Ili kufanikisha utekelezaji wa Sera hii kila taasisi inayohusika na dawa za kulevya itawajibika kutekeleza shughuli zilizopangwa katika mpango wa utekelezaji wa sera hii. Wahusika wa utekelezaji wa sera hii wataripoti kuhusu utekelezaji kulingana na viashiria na shabaha zilizopangwa kila mwaka. Wadau katika kuripoti watatumia mfumo wa ukusanyaji taarifa ambao utawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za hali ya dawa za kulevya nchini.

### 6.2 Tathmini

Matokeo ya utekelezaji yatafanyiwa Tathmini kila baada ya mwaka mmoja ili kusimamia na kuhakikisha kuwa mikakati iliyopangwa katika sera hii inatekelezwa kwa usahihi na uwazi. Ripoti ya ufatiliaji na tathmini itatolewa na kusambazwa ili kuwawezesha wahusika katika ngazi zote kuweza kubaini mafanikio, changamoto na kutoa maoni juu ya utekelezaji wa sera. Taarifa hizo zitakazoandaliwa zitatumika katika kufanya mapitio ya sera. Taasisi inayosimamia utekelezaji wa sera itaandaa fomu zitakazotumika katika ufuatiliaji na tathmni ya sera hii.

### 6.3 Mapitio

Mapitio ya Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya yatafanyika kila baada ya miaka mitano ili kubainisha hali halisi pamoja na changamoto zinazokabili masuala ya dawa za kulevya katika jamii. Hata hivyo, sera inaweza kufanyiwa marekebisho kila inapohitajika kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea katika utekelezaji wake.

### 6.4 Gharama na Rasilimali fedha

Wizara yenye dhamana ya masuala ya dawa za kulevya itaratibu utayarishaji wa muundo mahususi wa mahitaji ya kibajeti, ugawaji na ukusanyaji wa rasilimali, na kushirikiana na wadau wote husika na washirika wa maendeleo ili kufikia malengo ya utekelezaji. Jumla ya shilingi 16,956,000,000 Q ```zitahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa sera hii kwa kipindi cha miaka mitano.

Vigezo vifuatavyo vitazingatiwa kwa upangaji wa rasilimali za kifedha; vyanzo vya ufadhili, mashirika ya ufadhili, rasilimali watu, zana, vifaa vya utekelezaji, makadirio ya muda wa utekelezaji, gharama halisi zinazohitajika kwa utekelezaji.

### 6.5 Mkakati wa Mawasiliano

Wizara inayohusika na masuala ya dawa za kulevya itatayarisha Mkakati wa Mawasiliano kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ambao utajumuisha ubadilishanaji wa taarifa na mawasiliano, usambazaji wa nyaraka za Sera ya Dawa za Kulevya katika sekta zote, shabaha na malengo ya utekelezaji. Mkakati wa Mawasiliano utaoanisha juhudi za utekelezaji miongoni mwa taasisi za Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na Washirika wa Maendeleo. Mkakati huo utaundwa ili kuboresha utambuzi wa Kitaifa, Kikanda, na Kimataifa wa Sera ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, utasisitiza wajibu wa wadau wote na utaandaliwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili kuhakikisha ufikiaji wa watu wote.